# SURA YA 3

## MAMBO MUHIMU14 UNAYOPASWA KUYAJUA KUHUSU KUSUDI LA KUZALIWA KWAKO

***Kila mtu amezaliwa Kwa sababu/kuna kusudi la kuzaliwa,***

***Hakuna aliyezaliwa bila kusudi/sababu yoyote.***

Hakuna aliyezaliwa Kwa bahati mbaya, hata kama Mama yako alibakwa ndiyo ukazaliwa wewe, Ulizaliwa nje ya ndoa, ulizaliwa porini, Ulizaliwa na mama kichaa, Ulizaliwa na wazazi vipofu, Ulizaliwa na wazazi maskini n. k, kuna kusudi ndani yako ambalo umekuja kulitimiza hapa duniani. Yesu, Masihi alizaliwa kwenye zizi la ng'ombe, Uduni huo haukulipoteza kusudi lake, Luka 2:11-14 la kuokomboa ulimwengu kutoka kwenye dhambi.

**Kusudi lako si kwa ajili yako, ni kwa ajili ya watu, Kuna watu umetumwa uje uwakomboe, Usipolitimiza kusudi lako watu hao wataangamia.**

**Kusudi lako linaweza kuwa kwa ajili ya watu wote (Yeremia, alitumwa kuwa nabii wa mataifa, Yeremia 1:5) AU Kwa ajili ya kundi maalumu la watu (Samsoni alitumwa kwa ajili ya wanaIsraeli kuwakomboa kutoka mikononi mwa wafilisti, Waamuzi 13:1-5)**

**Kusudi lako ni maalumu kwa majira na nyakati maalumu (Mhubiri3:1), Si kila wakati linahitajika.**

Ester alizaliwa ili aje atimize kusudi lake wakati Hamani atakaponyanyuka kuwashambulia wana wa Israeli, (Soma kitabu cha esta), Wakati mwingine wote alikaa akisubiri wakati wake sahihi.

**Hakuna anayelijua kusudi lako Zaidi ya MUNGU (Aliyekupa kusudi}na wewe Mwenyewe.**

**Shetani hupata viashiria (meseji) juu ya kusudi la kuzaliwa kwako.**

Mwone Herode alivyotumiwa na shetani kipindi cha kuzaliwa Yesu Kristu, baada ya wale wamajusi kuiona nyota ya Yesu iking'aa **(MESEJI),** aliagiza watoto wote wakiume waliokuwa wamezaliwa kipindi kile wauawe, (Mathayo2:16-17)

Hii inaonyesha kuwa Shetani alipata meseji, akapanga mbinu za kulizuia kusudi lililokuwa limebebwa Na Yesu kwa kumtumia Herode.

**Shetani hayuko tayari kuona kusudi lako linatimia, kwani kusudi lako likitimia litampa pigo, Hivyo atatumia kila njia kuhakikisha kusudi lako halitimii.**

Ukubwa wa kusudi lako utaendana na vita atakavyoviinua juu yako (Mathayo 2:16-17, Waamuzi16:1-21)

**Usipolitimiza kusudi lako MUNGU atakuona mkaidi na atakuadhibu,**

Hata Kama ungekuwa wewe ungejisikiaje umemtuma, mwanao halafu asilete ulichomtuma**?**

**MUNGU anapokupa kusudi huwa anakupa pia NGUVU itakayokuwezesha kulitimiza kusudi Hilo,** NGUVU hiyo ni kipaji/Karama/Talanta /Uwezo wa kipekee kufanya jambo Fulani.

Samsoni alipewa nguvu nyingi za kimwili zitakazomsaidiakupambana wakati wa kulitimiza kusudi lake la kuwakomboa wana waIsraeli kutoka kwa Wafilisti (waamuzi 15:13-16)

Yeremia alipewa nguvu ya kunena/kuongea ili atimize vyema kusudi lake la unabii(Yeremia1:9-10)

**NGUVU iliyoko ndani yako(Kipawa/Talanta) haizuiliwi na chochote, Hata shetani na Majeshi yake hawawezi kuizuia**

**mkiingia kiwanja cha mapambano KUPAMBANA NAO (Live and Direct), Ili kupambana na Nguvu iliyoko ndani yako shetani hutumia njia zifuatazo(Indirectly):**

a. ***Anakupa upofu, Usilijue kusudi lako na usipolijua kusudi lako hautoijua nguvu yako na hata ukiijua nguvu yako atakufumba usilijue kusudi lako hivyo utaitumia nguvu yako kufanya jambo jingine ambalo si sahihi, kitendo ambacho kwake hakitampa mawazo(Stress) au kumwadhibu.***
b. ***Hukutumia wapelelezi(Explorers)wakupeleleze ili ajue siri za nguvu zako halafuakushambulie/akuangamize:***Kwa bahati mbaya sanawapelelezi hawa huwa watu wa karibu yetu mno, tunaowaamini na kuwapenda sana**, (wanaweza kuwa wazazi wetu, wenza wetu wa ndoa n.k)**

**Mfano:**

Samsoni alitumiwa Delila, Delila alikuwa kipenzi cha samsoni alimpeleleza samsoni mpaka akaijua siri za nguvu zake na wafilisiti wakamuangamiza. (Waamuzi 16:1-21)

***KUWA CHONJO, USITOE TAARIFA ZAKO OVYO OVYO***

***C.Hukutia hofu, kila mara unapofikiria kufanya jambo linaloendana na kusudi lako.***

Hujawahi kujuiuliza kwanini mara nyingi unapotaka kufanya vitu vyenye umuhimu mkubwa kwenye maisha yako roho yako husitasita kuliko unapotaka kufanya mabaya?

Shetani anapoona unataka kukitumia kilichoko ndani yako, anakutia hofu kuhakikisha hauchukui hatua yoyote.Kila wakati ukipata hofu KEMEA hilo ni pepo.

***KUMBUKA: FEAR IS devil/Hofu Ni shetani***

***D.Hukutumia mashambulizi*:** Hukutumia Watu wakukatishetamaa, wakusemevibaya, Wakutengenezee uzushi, wakutukane, Wakuangushe kwenye huduma, atakupadhiki, Magonjwa, ulemavu, Umaskinin.k) Lengo lake akupoteze kwenye njia ya kuzitumia nguvu zako na kulitambua kusudi lako.

**NGUVU hii ya kipekee hukutofautisha na watu wengine wote duniani (Key differentiator) na ukiitumia kufanya jambo lolote utafanikiwa, haswa ukiitumia kulitimiza kusudi lako.**

**Kila kitu kuhusu kusudi lako, kimeshaandaliwa tayari unachopaswa kufanya ni kulijua tu kusudi lako, Kuwa mwaminifu mbele za MUNGU na kuanza kuliishi.**

Samsoni alitumwa kuwakomboa wanaISRAELI kutoka mikononi mwa wafilisti ila hakujua ni kwa namna gani,

MUNGU alitengeneza njia ya kumuingiza samsoni katika eneo alilopaswa awepo ili alitimize kusudi lake. (Waamuzi 14:1-4)

Vivyo hivyo kwa Esta MUNGU alitengeneza namna ambayo Esta ataingia kwenye jumba la kifalme, Atakavyotimiza jukumu lake n.k

**Mafanikio ya kweli Ni kulitimiza kusudi lako la kuwepo duniani, Sio kuwa na pesa nyingi, magari ya kifahari, Elimu ya juu n.k**

*MAFANIKIO YAKWELI=KULITIMIZA KUSUDI LAKO=FURAHA+AMANI+UPENDO=UTAJIRI NA VITU VYOTE VILIVYOPO DUNIANI*.

**KUSUDI LA KUZALIWA HUWEPO KABLA YA MTU KUWEPO, YAANI KABLA HATA YAKUZALIWA. (PRE-EXISTED)**

Unakumbuka nabii Yeremia alivyoambiwa na MUNGU kipindi anaambiwa kusudilake?( Yeremia1:4-5)

*Neno la bwana lilinijia, kusema, Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua na kabla ya kutoka tumboni, nalikutakasa, Nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.*

Kabla sijakuumba nalikujua, Hakumjua Yeremia Kama mtu alimjua Yeremia Kama kusudi,